East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

SIMULIZI ZA UNYANYAPAA UNAOHUSIANA NA VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI NCHINI KENYA KIBAADAUSASA

Alexander K. Rotich,

Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030, Kericho, Kenya, alexanderotich@gmail.com

Article history:

Received: 2 Dec 2018
Revised: 18 Jan 2019
Accepted: 15 Feb 2019
Published: 21 Feb 2019

Keywords:

Nyimbo,
Unyanyapaa,
VVU/UKIMWI,
Kiswahili,
Baadausasa.

IKISIRI

Tangu kuibuka kwa janga la Virusi Vya Ukimwi/Ukimwi maarufu kama VVU/UKIMWI zaidi ya miongo mitatu iliyopita, juhudi nyingi zilizowekwa na serikali za mataifa mbalimbali, masharika yasiyokuwa ya kiserikali na watu binafsi hazijafaulu kutokomeza kabisa janga hili. Hii ni kwa sababu, kama magonjwa mengine hatari, ugonjwa huu unahusishwa na unyanyapaa unaoelekezwa kwa walioambukizwa Virusi Vya Ukimwi. Isitoshe, hata matumizi ya dawa za kupunguza makali ya virusi husika, almaarufu ARVs yamekuwa chanzo kikubwa cha unyanyapaa badala ya kuleta afueni kwa waathiriwa. Unyanyapaa unaoelekezwa kwa wanaoonyesha dalili za kuambukizwa Virusi Vya Ukimwi pamoja na wale wanaotumia dawa za kupunguza makali unaelekea kuufanya ugonjwa huu kuwa changamano zaidi. Kwa kujikita katika nyimbo tatu za Kiswahili zilizoimbwa katika nyakati hizi za kibaadausasa, makala hii imepania kubainisha na kufafanua simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo zinazokuza na zinazopinga unyanyapaa unaohusishwa na VVU/UKIMWI. Kwa kuongozwa na nadharia ya Baadausasa, watafiti walibainisha na kuchanganua vipande vya simulizi zinazohusiana na unyanyapaa husika. Aidha, wamedhihirisha kuwa, nyimbo, hasa za kibaadausasa ni chombo mhususi kinachoweza kutumiwa na wanajamii kupiga vita unyanyapaa unaohusishwa na VVU/UKIMWI hasa ikizingatiwa kwamba, mbali na kutatiza ufanisi uliofikiwa katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI, unyanyapaa ndio chanzo cha vifo vingi vinavyohusishwa na VVU/UKIMWI.

UTANGULIZI

Janga la Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI limewahangaisha binadamu kote ulimwenguni kwa zaidi ya miongo mitatu mpaka sasa. Ugonjwa huu ni hatari na unahusishwa na suala la ngono na hivyo kuzua simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo zinazoelekea kukuza na kupinga unyanyapaa unaohusishwa na walioambukizwa mtawalia. Hii ni kwa sababu walioambukizwa walichukuliwa kuwa wapenda anasa, starehe na uasherati. Kwa jinsi hii, hata wale walioambukizwa kupitia njia nyingine kama vile kupewa damu isiyo salama, na kudungwa au kujidunga sindano zisizosafishwa waliishia kubaguliwa licha ya kutoshiriki ngono za kiholela.

Kugunduliwa kwa dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya UKIMWI almaarufu ARVs kulileta

matumaini makubwa kwa wale waliokuwa wameambukizwa. Hata hivyo, matumizi ya dawa hizi yaliibua changamoto nyingine ya unyanyapaa. Hii ni kwa sababu walioonekana wakizitumia dawa hizo walitengwa na kubaguliwa na wanajamii. Sababu ya kubaguliwa huku ni kuwa, watumiaji wa dawa za kupunguza makali ya VVU, kwanza walikuwa waasherati machoni mwa wanajamii na ndiyo maana wakaambukizwa. Pili, walioambukizwa na hivyo kutumia dawa husika walibaguliwa kwa sababu walichukuliwa kuwa wanaishi huku wamekufa au wamekufa huku wanaishi. Aidha, walichukuliwa kuwa wanakufa polepole kwa sababu wanajamii walichukulia VVU kuwa hukumu ya kifo kwa walioambukizwa.

Kwa kujikita katika nyimbo tatu za Kiswahili za nyakati hizi za kibaadausasa nchini Kenya, makala haya yanalenga kubainisha na kujadili simulizi kuu zinazoelekea kukuza unyanyapaa unaohusishwa na VVU/UKIMWI na vile vile simulizi ndogo ndogo zinazopinga unyanyapaa. Nyimbo zilizoteuliwa ni: *Nimeupata Vipi?* wake Daddy Faddy, *Vuta Pumzi* wa Longombas na *Starehe* wa Ferooz na Prof. Jay.

Mapitio ya Maandishi

Unyanyapaa una maana tofauti tofauti kwa watu tofauti tofauti. Goffman (1974) anaeleza kuwa unyanyapaa ni sifa ya kuaibisha na ambayo humfanya mtu aonekane mwenye doa na hivyo anayefaa kuadhiriwa kulingana na mielekeo iliyokita katika jamii. Anaendelea kueleza kuwa asili ya neno hili ni Ugiriki ambapo lilikuwa na maana ya chale aliyowekwa mtu kwa kufanya kitendo cha kuhatarisha au cha kuponza. Madhumuni ya alama hiyo ilikuwa ni kumtambulisha mtu aliyekuwa na dosari, ila au waa. Stein (2010) anaeleza kuwa, kadri muda ulivyoendelea, istilahi hii ilifungamanishwa na ukengeushi pamoja na tabia zisizokuwa za kawaida hasa zinazoleta hisia hasi hususan kutowajibika kingono.

Kulingana na Kamusi ya TUKI (2010) unyanyapaa ni fedheha au mtwezo unaohusishwa na chochote kisichokubalika katika jamii. Ni hali ya kuwepo kwa hisia za "sisi na wao" ambapo watu walionyanyapaa wanatiwa alama ya kuwafanya kuwa tofauti na wanajamii wengine na kulaumiwa kwa ajili ya tofauti hiyo.

Katika jamii zetu kwa mfano, watu wengine wanaposikia kuwa mtu ana Virusi Vya UKIMWI, humwona kama mtu anayekufa polepole au aliyekufa huku akiishi. Awali, mtu wa aina hii hangeguswa au kugusana na mwingine asije akawaambukiza. Hii ni kwa sababu UKIMWI ni ugonjwa ambao huwaogofya watu wengi hasa kutokana na kutopata habari zilizo sahihi kuuhusu. Aidha wanajamii wengi huwa na hisia pendelevu au hasi juu ya UKIMWI.

Aina za Unyanyapaa

Ubaguzi dhidi ya watu walio na VVU/UKIMWI huchukua sura mbalimbali ambazo ni pamoja na kukataliwa, kubaguliwa, kutengwa, kuwakwepa walioambukizwa, kuchunguzwa damu bila kujuzwa, kukosa kuweka siri au kutangaza hali ya UKIMWI ya mtu, kuingiliwa kwa nguvu au bila kuzingatia sheria, kuwekwa karantini na kunyimwa urithi mtu anapofiwa (*mobile.aidsmap.com*). Vurugu zinazofungamanishwa na unyanyapaa au hofu ya kuingiliwa kwa nguvu huwazuia watu wengi kujichunguza, kurudi kuchukua matokeo au kupata matibabu na hivyo kugeuza ugonjwa hatari ambao ungetibiwa kuwa hukumu ya kifo na kukuza kuenea kwake.

Kuna aina nne za unyanyapaa unaofungamanishwa na VVU/UKIMWI.:

i. Unyanyapaa wa kiufugamano au kiuhusika. Huu ni unyanyapaa unaofungamanishwa na ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Ni akisiko la hofu inayohusishwa na ugonjwa wowote hatari na wa kuambukizana.
ii. Unyanyapaa wa kimfumo au kiishara. Huu ni unyanyapaa unaotumia UKIMWI kueleza mielekeo kuhusu makundi fulani ya kijamii yanayohusishwa na ugonjwa wenyewe.
iii. Unyanyapaa wa kifadhila au kiustahiki. Huu ni unyanyapaa unaoelekezwa kwa watu kama vile makahaba na matajiri wanaohusishwa na suala la VVU/UKIMWI au watu walioambukizwa VVU.
iv. Unyanyapaa wa kibinafsi. Huu ni unyanyapaa unaoendelezwa na mtu aliyeaambukizwa dhidi ya nafsi yake baada ya kugundua ameambukizwa. Ni unyanyapaa unaomfanya mgonjwa

ajitenge na wanajamii wengine. Wataalamu wa afya niliowahoji wanadai kuwa, huu ni unyanyapaa unaosababisha vifo vingi zaidi vinavyohusiana na VVU/UKIMWI.

Aghalabu, unyanyapaa au ubaguzi unaohusiana na VVU/UKIMWI huelezwa mintaarafu ya aina moja ya unyanyapaa au zingine hasa zile zinazohusishwa na mabasha, wafanya ajira ya ngono, wanaotumia mihadarati ya kujidungia, wazinzi, huntha na kadhalika. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba, unyanyapaa hupelekea watu kutochukuliwa kwa hadhi na heshima zinazohusiana na ubinadamu. Kufedheheshwa, kubaguliwa au kutengwa aghalabu huwa sehemu mbaya zaidi ya maisha kwa wale walio na VVU/UKIMWI. Wengi husema: "Siwezi kugeuka na kuwaambia nina VVU/UKIMWI kwa sababu ninajua watakavyonichukulia". Haya ni mawazo yanayopingwa na wanabaadausasa.

Matokeo ya Unyanyapaa

Matokeo ya unyanyapaa ni kutukanwa, kukataliwa au kutengwa, kufitiniwa na kutoshirikishwa katika shughuli za kijamii kwa walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Hofu juu ya tabia hizi huwafanya watu walio na Virusi Vya UKIMWI kuogopa au kuwa na mfadhaiko wa kutangaza au kufichua hali yao ya VVU/UKIMWI. Aidha huwafanya kukwepa kujumuika na watu wengine. Hali hii huenda ikawafanya wateseke katika unyamavu badala ya kufaidi msaada wanaouhitaji. Isitoshe, unyanyapaa huwafanya watu wasadiki yanayosemwa na watu wengine kuhusiana na VVU/UKIMWI. Mathalan, wanaweza kuamini kuwa VVU/UKIMWI ni hukumu ya kifo kwao au kuwa wote walio na UKIMWI ni wazinzi au wasiowajibika.

Tokeo moja la unyanyapaa kwa mujibu wa Mutembei (2009) ni kukimbiwa kwa wagonjwa wa UKIMWI kwa kuhofia kuambukizwa. Katika hali hii, waathiriwa huachwa bila msaada wa maana. Jambo hili lilikuwamo katika jamii tangu zamani kwani watu wliogopa magonjwa sugu. Maoni haya ya Mutembei yanaoana na yale ya Wolfgang (1997) yanayoonysha kuwa, kutengwa kwa wagonjwa kulifanyika ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa sugu kwenye kambi za wafungwa wa Kiyahudi kule Ujerumani.

Mnamo miaka ya 1920, ugonjwa wa malale na ndui uliwafanya wenyeji kutenga wagonjwa katika vijiji vyao au kuwakimbia kabisa (Roberts, A.D, 1986). Kwingineko, magonjwa kama vile ukoma na magonjwa mengine ambayo watu walihofia kuambukizwa yaliwafanya wagonjwa kutengwa.

Kuhusiana na kuwatenga wagonjwa wa UKIMWI kulianza 1992 kule Marekani wakati aliyekuwa anawania kiti cha useneta alipopendekeza kuwa wagonjwa wote wa UKIMWI wazuiliwe huku akipinga kutolewa kwa fedha za utafiti wa kutibu ugonjwa huo (http://www. huffingtonpost.com /2007/12/08/huckabee-wanted-AIDS-quar_n_75924.html). Naye Randy Shilts (1987) anasema kuwa miaka ya mwanzo ya themanini kule Marekani damu ya mashoga ilitengwa isitumike na watu walioihitaji. Mashoga walionana jambo hili kuwa mwanzo wa kuwatenga hata wao. Jambo hili lilizidisha unyanyapaa kwa wgonjwa wa UKIMWI.

Tokeo lingine la unyanyapaa ni kuwahukumu wagonjwa wa UKIMWI kwa watu kuwapa majina ya kuwaondolea utu. Jamii iliwahukumu wagonjwa husika kwamba walipata ugonjwa kwa sababu walikuwa waosaji. Walioenekana kama watu wasiostahiki kuitwa watu. Hukumu hii ilichochewa zaidi na taasisi za kidini. Wanajamii ambao walifuata mkumbo wa kidini au waliokosa uelewa wa kina kuhusu UKIMWI walitumia lugha ya kuhukumu na hivyo kukatisha tamaa.

Kulingana na *mobile.aidsmap.com*, unyanyapaa aghalabu hufungamanishwa na vitu au hali zinazoogofya. Kwa mfano, tangu kuripotiwa kwa kesi za kwanza za ugonjwa huu katika miaka 1980s, watu walio na UKIMWI wamekuwa wakifedheheshwa kwa sababu:

i. UKIMWI ni hatari; ni ugonjwa unaotishia maisha au uhai na hasa ikizingatiwa kuwa, kuna historia ndefu ya kufedheheshwa kwa wagonjwa wa Saratani, Kifuakikuu na Ukambi.

ii. Watu wasiojua namna Virusi Vya UKIMWI vinavyoambukizwa huhofia kuambukizwa kupitia mitagusano ya kijamii.

iii. Watu wengine wana mitazamo au misimamamo mikali kuhusu kitendo cha

ngono. Wenye misimamo kama hii huchukulia kuwa, kuna nyakati na miktadha ambamo ni hatia au kosa ama watu fulani hawafai kuwa na tabia fulani fulani.

iv. Fikra za watu kuhusu UKIMWI hutegemea namna wanavyochukulia makundi ya kijamii yanayoathirika zaidi kutokana na ugonjwa huu. Wengine tayari wana hisia hasi kuhusu wanawake, mabasha, watu weusi, watumizi wa dawa za kulevya na kadhalika. Hisia hizi za 'sisi' na 'hao' zinadhihirika katika nyimbo tulizozichanganua.

Maana ya simulizi kuu na simulizi ndogo.

Simulizi kuu ni simulizi zinazopatikana katika jamii na ambazo inapania kufafanua maana kila kitu kama vile maana ya uhalisi, hali ya binadamu; maana ya maisha ya mtu binafsi na jamii nzima kwa jumla, malengo ya maisha haya na mbinu zinazowezesha kufikiwa kwa malengo haya. Ni 'Nadharia za kila kitu' ambazo hufafanua siyo tu hali halisi wakati huu bali pia huangazia wazo kuu linalotarajiwa na ambalo halijatimia. Kwa ufupi, simulizi kuu ni maelezo yaliyozoeleka na wanajamii kuhusu jambo, kitu au hali fulani.

Simulizi ndogo ndogo nazo ni zile ambazo hutoa maelezo kuhusu ukweli fulani katika maisha ya wanajamii. Hutoa maelezo kuhusu maisha ya kila siku; maelezo ambayo hayatolewi na simulizi kuu. Kwa jinsi hiyo basi, simulizi ndogo hukinzana na simulizi kuu na wakati mwingine hujikinza zenyewe. Mathalani, katika fasihi andishi, pale ambapo simulizi kuu inasisitiza usomaji wa riwaya uanzie mwanzo kwenda katikati na kisha hitimisho ili kudumisha ushikamo, simulizi ndogo ndogo hupendekeza kuwa, usomaji huu unaweza kuanzia popote. Msomaji anaweza kuanzia mwanzo kwenda mwisho kisha kumalizia katikati au aanzie katikati aende mwisho na kumalizia mwanzo. Aidha, msomaji anaweza kuanzia mwisho kuelekea mwanzo na kisha kumalizia katikati. Mitindo hii ya usomaji husababisha kukosekana kwa ushikamano, hali inayosherehekewa na simulizi ndogo ndogo na kusikitikiwa na simulizi kuu. Katika sehemu inayofuata, tunabaisha simulizi zinazohusishwa na VVU/Ukimwi katika nyimbo zilizoteuliwa kwa ajili ya makala haya.

Simulizi kuu na Simulizi ndogo Zinavyodhihirika katika Nyimbo zilizoteuliwa.

Tunaanza na wimbo *Nimeupata Vipi?* Ulioimbwa na Daddy Faddy. Kwanza kabisa, mhusika analia anapoanza kukonda na kuwa na upele mwilini; dalili zinazochukuliwa na wanajamii kuwa za Virusi Vya Ukimwi. Aidha, anaeleza kuwa amepimwa na kuambiwa kuwa amaeathirika. Anashangaa vipi ameathirika ilhali hajawahi kufanya ngono au uasherati. Isitoshe, anawaomba wanajamii wasimtenge kwa kuwa hakupata ngoma kutokana na zinaa. Tazama mistari inayofuata ya wimbo huu:

1. *Nilivyokonda majibu niliyopewa yanitisha*
2. *Nimeambiwa kwamba nimeathirika*
3. *Wakati ngono sijawahi kufanya*
4. *Mi naomba msijenitenga*
5. *Kwa sababu nimeathirika*
6. *Mbona Faddy Daddy unazidi konda?*
7. *Mwili mzima umejaa upele*
8. *Kama hivyo twende zetu Tanga*

Kutokana na mistari ya 1 hadi wa 8 hapo juu, simulizi kuu ni kwamba, njia ya pekee ambayo kwayo mtu hupata maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi ni kushiriki. Aidha yeyote aliyekonda na kuwa na upele mwilini huchukuliwa kuwa ana VVU. Isitoshe, mtu kama huyo anafaa kutengwa. Tazama mstari wa 4 na 8.

Simulizi ndogo ndogo zinazopinga simulizi kuu na hivyo kupinga unyanyapaa katika wimbo huu zinadhihirika pale ambapo mhusika anateta kwamba hakupata virusi kwa kushiriki uasherati na kwamba alijilinda sana. Anawaomba wanajamii wasimtenge kwani huenda aliambukizwa kupitia damu aliyoongezewa au kupitia kwa ala zinazotumiwa kwenye saloni anakokwenda kunyolewa. Tazama mistari ifuatayo:

9. *Sikupata ngoma sababu ya zinaa*
10. *Wapi UKIMWI nimeupata?*
11. *Ama kwa matanga nilipoongezewa damu?*
12. *Ama kwenye saloni kwenye kunyoa?*

Kwa hivyo simulizi ndogo ndogo zinazobainika katika wimbo ni kwamba, ngono si njia ya pekee ya kuambukizwa VVU. Mtu anaweza kuambukizwa kupitia kwa njia nyingine kama vile kuongezewa damu isiyo salama au kwa kutumia ala zenye

makali kwa ushirika. Simulizi ndogo ndogo nyingine ni kwamba, walioambukizwa hawapaswi kutengwa kwa misingi ya kuwa na virusi. Kuwafanyia hivyo ni kuwahukumu kwamba ni waasherati.

Hali kama hii inadhihirika katika wimbo wimbo Vuta Pumzi uliosanifiwa na Longombas. Katika wimbo huu, simulizi kuu zinazohusiana na unyanyapaa zinabainika kupitia kauli za waimbaji wanaowatahadharisha wasikilizaji kwamba wajichunge na warembo wenye marasa wenye mapaja na weupe. Aidha, wanawaonya waepukane na wanaume wenye vifua, warefu na wenye nguvu. Wanasema kuwa, kijuujuu wanaonekana wazuri; ni wazuri kinyama. Ingawa wanaonekana wenye afya, pengine wana mdudu na wanatuacha. Aidha, kutokana na mijadala katika makundi, tulibainisha kuwa kitendo cha kuchora kinamaanisha kuandika wosia kwani Ukimwi unachukuliwa kuwa hukumu ya kifo. Ni wazi kuwa, hizi ni simulizi zinazokuza unyanyapaa kwa sababu ya baadhi ya watu kushukiwa na wanajamii kuwa na virusi na kwamba wanaishi huku wanakufa au wamekufa huku wanaishi. Longombas wanaimba:

13. *Jamani nisikilizeni, mnisikilize*
14. *Kuna wanawake warembo, wenye marasa, na mapaja, weupe*
15. *Ni wazuri kinyama*
16. *Kuna wanaume wengi*
17. *Wenye vifua, na warefu, na wenye nguvu*
18. *Ni wazuri kinyama*
19. *Lakini tujichunge*
20. *Pengine wanao mudu*
21. *Wanatuacha, wana-go*
22. *Usimwone amejaza nyuma ukadhani ako poa.....*
23. *Pengine anatuacha, kesho anachora.*

Mbali na kudhihirisha simulizi kuu, wimbo huu pia unadhihirisha simulizi ndogo ndogo zinazopinga simulizi kuu kwamba, mtu akiambukizwa Virusi Vya Ukimwi maisha yake yamefika tamati. Waimbaji wanawahimiza walioambukizwa wasitamauke kwani Ukimwi ni kama ugonjwa wowote mwingine kama vile Malaria, yaani Ukimwi si hukumu ya kifo namna wanajamii wanavyouchukulia. Wanashauri kuwa mwathiriwa akimeza dawa, afanye mazoezi na kuzingatia lishe bora ataendelea na maisha yake kama kawaida. Simulizi hizi ndogo ndogo zinadhihirika katika mistari inayofuata:

24. *Na kama unao, si mwisho wa maisha*
25. *Ni ugonjwa tu kama malaria*
26. *Meza dawa, piga tisi, kula vizuri utaishi fiti*
27. *Maisha utayasukuma*.

Wimbo wa tatu ambao simulizi zake zilichanganuliwa kwenye makala haya ni Starehe ulioimbwa na Ferooz na Profesa Jay. Simulizi kuu inayotangulia kudhihirika ni kwamba, aliyeambukizwa VVU huishia kujilaumu, kujuta, kutamauka na hata kujitenga na wanajamii wengine kwani haoni matumaini ya kupona tena na ndipo anaanza kuwaaga. Aidha simulizi nyingine kuu ni kuwa, mtu aliyeathiriwa humlaumu shetani mbali na kujilaumu yeye mwenyewe. Kwa jinsi hiyo huanza kuendeleza unyanyapaa dhidi ya nafsi yake. Pamoja na hayo, kukonda, mwili kujaa vidonda, kutapika na kunyonyoka kwa nywele kuchukuliwa kuwa dalili za ugonjwa wa Ukimwi peke yake ni simulizi kuu miongoni mwa wanajamii. Dalili hizi huwafanya washuku na hata ajishuku yeye mwenywe. Wasanii wa wimbo huu waimba hivi katika mistari ifuatayo:

28. *Sasa hapa mimi nipo kitandani*
29. *Kupona mimi tena haiwezekani*
30. *Sasa najuta mwenzenu*
31. *Dokta cheki nilivyokonda*
32. *Mwili umetapakaa vidonda*
33. *Kukohoa, kutapika.....*
34. *Ona hata nywele zilivyonyonyoka*
35. *Hii yote dalili zote za umeme*
36. *Ibilisi amefaulu kunivuta*
37. *Sasa sijui wa kumlaumu nani*
38. *Kati ya nafsi yangu na shetani.*
39. *Kwaherini kwaherini.....*

Wimbo huu pia una simulizi ndogo ndogo jinsi zilivyo nyimbo mbili zilizotangulia. Mathalani, pale ambapo simulizi kuu inaeleza kuwa, mtu anaweza kuambukizwa virusi kwa kufanya ngono na washirika wengi na bila kutumia kondomu, simulizi ndogo ndogo hueleza jinsi wahusika wanavyotekeleza kitendo hicho na kutoa sababu za kutozingatia matumizi ya kondomu na hivyo kusawiri hali halisi ya matukio ya kila siku.

Katika wimbo huu basi, simulizi ndogo ndogo zinadhihirika pale mwathiriwa anapotoa msururu

wa wanawake aliofanya ngono nao. Kwa mfano, anaeleza kwamba, alimwendea huyu akimrudia yule. Aidha, anaeleza kuwa, saa saba ameachana na Jacky, sasa ako na Salama na saa kumi na mbili ana miadi na wengine wawili. Isitoshe, atafunga siku kwa kukutana na Lily saa mbili usiku, almuradi aliishia kuwabadilisha wanawake wengi wachanga kwa wakongwe. Mhusika pia anatoa sababu ya kutotumia kondomu, kwamba matumizi yake yangepunguza ladha ya mapenzi. Ingawa hali hii inaonekana kupigwa chuku, mtazamo wa kibaadausasa ni kwamba, huu ni uhalisi jinsi ulivyo; uhalisi ambao hauelezwi na simulizi kuu. Simulizi kuu haiwezi kutoa orodha ya wanawake au kutoa sababu za kutotumiwa kwa kondomu.

Mfano mwingine ni kuwa, simulizi kuu huchukulia dalili za kukonda, ukurutu wa ngozi, kukohoa kuwa dalili za Ukimwi bila kueleza kwamba zinaweza kuwa dalili za magonjwa mengine. Kwa kufanya hivi simulizi kuu zinakuza na kuendeleza unyanyapaa. Aidha, simulizi kuu hueleza tu kwamba kukohoa ni dalili mojawapo ya Ukimwi. Simulizi ndogo ndogo hubainisha hali halisi ya kukohoa kwa aliyeambukizwa, kwamba akohoa mara sitini na mbili kwa siku.

Isitoshe, wasanii wanatoa simulizi ndogo ndogo zinazopinga simulizi kuu kwamba, kukonda ni dalili ya kuambukizwa VVU pekee yake pamoja na zile zinapinga simulizi kuu inayodai kuwa Ukimwi ni hukumu ya kifo, na hivyo kupinga unyanyapaa unaoendelezwa dhidi ya walioambukizwa pamoja na wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU. Mistari inayofuata kutoka kwa wimbo Starehe inashereheshea simulizi hizo ndogo ndogo tulizofafanua hapo juu. Tazama mistari yenyewe:

40. *Nilibadili mademu kama vidaladala*
41. *Saa saba nikiona, nimeachana na Jacky*
42. *Sasa napata Salama*
43. *Saa kumi na mbili, nina appointment na madame wawili*
44. *Achana na Lily, tutakutana saa mbili*
45. *Ubaya ni kwamba, condom sikuitambua*
46. *Kwa kujua kwamba ladha ya mapenzi ingepungua*
47. *Idadi ya wanawake ikawa lukuki*
48. *Usikate tamaa*
49. *Unaweza ukakonda kwa Typhoid au TB*
50. *Kula vizuri, fanya mazoezi, pumzisha mwili wako*
51. *Ukizingatia hayo, utaishi kwa matumaini*
52. *Sasa jaribu, muda bado unao.*

Hitimisho.

Nyimbo zilizochanganuliwa katika makala haya zimekitwa katika muktadha wa kibaadausasa. Katika kuzichanganua nyimbo hizi, tumeonyesha kwamba, zimesheheni simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo ambazo zinaweza kukuza au kudumaza unyanyapaa unaohusishwa na Virusi Vya Ukimwi pamoja na ugonjwa wenyewe wa Ukimwi. Vile vile, tumebainisha kwamba, simulizi kuu aghalabu hutuonyesha kile ambacho kimezoeleka na wanajamii. Aidha, hii ni simulizi ambayo inaelekea kukuza na kuendeleza unyanyapaa unaohusishwa na Ukimwi. Isitoshe, tumedhihirisha kwamba, katika nyimbo za kibaadausasa,kuna simulizi ndogo ndogo ambazo zinakinzana na simulizi kuu na hivyo kupinga au kudumaza unyanyapaa unaoenelezwa dhidi ya walioambukizwa VVU, wale wanaogua ugonjwa wa Ukimwi na wale wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU.

Marejeleo

Goffman, E. (1974). Frame Analysis: An Assay on the Organization of Experience. New York: Hamper and Raw.

Mutembei, A.K, (2009). UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2006. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar-es-salaam.

Roberts, A.D(mhr) (1986). The Cambridge History of Africa.Vol. 7 from 1905-1940. Cambridge University Press. Cambridge.

Shilts, R. (1987). And the Band Played on: Politics, People andthe AIDS Epidemic. St. Martins Press, New York.

Stei, J. (2010). HIV/AIDS Stigma. The Latest Dirty Secret. African Journal of Aids Research 2(2), 95-101.

TUKI (2010). Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar-es-salaam.